

MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MACHI, 2018 NA MWELEKEO WA APRILI, 2018

Dondoo za Aprili, 2018

Taarifa hii inatoa muhtasari wa hali ya viashiria vya hali ya hewa na mwenendo wa mvua katika mwezi wa Machi, 2018 na mwelekeo wa viashiria na hali ya mvua kwa mwezi Aprili, 2018 nchini.

- a) Mvua za *'Msimu'* katika maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2018.
- b) Mvua zinatarajiwa kuendelea kunyesha katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua hususan wiki mbili za kwanza za mwezi, isipokuwa maeneo ya Nyanda za juu kaskazini mashariki ambapo vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa.

1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI, 2018 NA MATAZAMIO KWA MWEZI APRILI, 2018.

1.1 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI, 2018

Wiki tatu za mwanzo za mwezi Machi, mvua za *'Masika'* na *'Msimu'* zimekuwa za kuridhisha katika maeneo mengi ya nchi, upungufu wa mvua umeonekana katika maeneo mengi ya nchi katika wiki ya mwisho ya mwezi Machi.

2.0 MATAZAMIO APRILI, 2018

2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la kati la Kitropikali la bahari ya Pasifiki pamoja na eneo la Pwani ya Angola, hata hivyo joto la juu ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi, ambapo hali ya joto la wastani inatarajiwa katika pwani ya Somalia. Hali hii ya mifumo inatarajiwa kuchangia kuwepo kwa mvua za wastani katika maeneo mengi ya nchi.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA MWEZI APRILI, 2018

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vingi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo

hususan katika wiki ya kwanza na ya pili, ikifuatiwa na upungufu wa mvua wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Upungufu wa mvua unatarajiwa katika maeneo mengi katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi, ikifuatiwa na Ongezeko la mvua katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2018.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): Vipindi vingi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi April, ikifuatiwa na upungufu wa mvua katika wiki mbili za mwezi zilizosalia.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vingi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi April, ikifuatiwa na upungufu wa mvua katika wiki mbili za mwezi zilizosalia.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Mvua za wastani zinatarajiwa katika kipindi cha mwezi Aprili, 2018.

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa, Mbeya pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro): Vipindi vingi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususan wiki mbili za mwanzo wa mwezi, zikifuatiwa na mvua za wastani katika maeneo mengi wiki mbili za mwisho.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vingi vya mvua vinatarajiwa hususan katika wiki mbili za mwanzo za mwezi Aprili, ikifuatiwa na upungufu wa mvua katika kipindi kilichosalia.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Vipindi vingi vya mvua vinatarajiwa hususan katika wiki mbili za mwanzo za mwezi Aprili, ikifuatiwa na upungufu wa mvua katika kipindi kilichosalia.

Imetolewa na;

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA